# SURPRISE YA AIBU - 01

Mazoea kwa kweli ni ugonjwa pamoja na kuwa na kila kitu katika maisha yangu hakuna nilicho kikosa. Nilikuwa na maisha mazuri watoto wangu wote wana maisha mazuri, lakini tabia zangu mbaya ambazo nilishindwa kuziacha ndizo zilizonifikisha hapa. Nilitamani dunia ipasuke kwani ilikuwa aibu ya mwaka mbele ya watoto wangu. Pamoja na kufanya za Siri lakini leo nimeumbuka mbele ya wanangu, nasema Mimi tena basi.

****

Simu iliendelea kulia Martin aliacha gezeti na kuichua, alipoangalia namba zilikuwa za mdogo wake anayeishi Canada aliipokea
"Haloo Edna leto story mdogo wangu."
"Shikamoo kaka."
"Marahaba, za Otawa?"
"Nzuri, sijui za huko Bongo?"
"Za huku safi, mbona kimya?"
"Si mimi nyie ndiye uliye nisusa."
"Tuachane na hayo siku zote upigapo simu huwa una jipya."
"Ni kweli kaka"
"Ehe lete story."
"Kaka ni hivi jana nimempigia asimu mama lakini sikumpata nilitaka nimualifu yeye kwanza ndio niwataalifu nyinyi kaka zangu, vipi na Moses hajambo?"
"Mmh! Yule kaka yako mtu wa safari si mnajua kazi za serikali kila kukicha anazunguruka na mheshimiwa."
"Basi ina maana hata kwa mama hamjaenda muda mrefu?"
"Ni kweli, kwa upande wangu nina mwezi sasa."
"Aah! Jamani mama yetu ni mmoja inatakiwa tuwe tunamtembelea hasa nyinyi uliye karibu."
"Ni kweli, shughuli zimetubana lakini nilipanga wiki ijayo niende kwa bi mkubwa."
"Sasa ni hivi mimi nilikuwa nipo njiani kuja huko."
"He! Mbona ghafla kuna nini?"
"Aah! Kaka kuja nyumbani mpaka pawepo na kitu, kwa mama yetu ni muhimu hata kila siku kumuona. Nampenda sana mama yangu na nikiolewa naondoka naye."
"Yaani wewe ndiye mwenye mapenzi kuliko watoto wake wote?"
"Nyinyi mpo karibu lakini mwezi unapita bila kumtembelea bi mkubwa."
"Edna tuachane na hayo ulikuwa unasemaje mdogo wangu?"
"Ni hivi kaka yangu, huku nimepata mchumba ambaye yupo tayari kufunga ndoa na mimi."
"Hongera, ni raia wa nchi gani?"
"Ni Mkanada mwenye asili ya Afrika."
"Mmh! Haya, sasa ulikuwa unasemaje?"
"Tumekubaliana mimi nitangulie kuwajulisha kisha yeye atafuata, sijui kwa hilo mnasemaje kaka yangu?"
"Siyo baya sasa unakuja lini?"
"Wiki ijayo."
"Itakuwa vizuri maana nina imani tutakutana kwa mama."
"Basi mjulishe na kaka Moses."
"Basi unganisha mawasiliano ya watu watatu ili tulizungumze kwa pamoja."
Edna aliunganmisha mawasiliano ya watu watatu na kuanza kuzungumza na kaka yake Moses ambaye anamfuata kwa mara ya pili ambaye alikuwa katibu mkuu ofisi ya Rais.
"Haloo kaka."

"Ooh! Bibi za Canada?"
"Nzuri tu kaka, shikamoo"
"Marahaba, naona leo umenikumbuka mdogo wangu."
"Nitafanya nini na ninyi mmenisusa."
"Hapana mdogo wangu kazi za serikali nimenibana ila nitatulia tu."
"Haya kaka,  za misafara maana nasikia kila alipo rais na wewe upo."
"Nitafanyaje na mimi nimeichagua hii kazi."
"Vipi upo wapi kwa sasa?"
"Nipo Denmark."
"Mmh!" Edna aliguna.
"Mbona una guna ulikuwa unasemaje?"

Edna anamueleza yote kama aliyomueleza kaka yake mkubwa Martin na jinsi walivyo panga kukutana kwa mama yao wiki ijayo.

"Kumbe ni hivyo, hakijaharibika kitu mdogo wangu, wiki ijayo nitakuwa Tanzania na nitakuwa na mapumziko marefu ya wiki tatu kwa hiyo safari ya kwenda kwa mama tutakuwa pamoja."
"Wawooo, itakuwa bonge la Surprise," Edna alifurahishwa na maneno ya kaka yake.
"Sasa ni hivi tusimjulishe mama tumzukie bila yeye kujua akiamka asubuhi atukute mlangoni kwake hiyo unasemaje?"
"Si mchezo ni Bonge la Surprise," Edna aliunga mkono.
"Kwa hiyo wote tukutane kwa bwana mkubwa Arusha siku moja kabla ya kwenda kwa mama."

Walikubaliana wote watatu ambao ni watoto wa mama mmoja lakini hawakubahatika kumuona baba yao. Baada ya kuelezwa na mama yao kuwa baba yao alimkimbia na kumuachia watoto. Mama yao ambaye aliwalea watoto wake na kufaniwa kuwasomesha iliyo ya juu, ambao baada ya masomo kila mmoja alipata kazi nzuri.

Historia ya maisha ya mama yao iliyowafikisha pale, iliwafanya watoto wake wamlee mama yao kama mboni ya macho yao. Kuonesha wanamjali mama yao  walimjengea mama yao jumba la kifahari sehemu za Mbezi na kumuwekea wafanyazi pamoja na magari ya kutembelea.

Kila mmoja alikuwa na hamu ya kukaa na mama yake, lakini aliwakatalia kwa kusema kila mtu aishi maisha yake ili mwenye hamu afunge safari kumfuata.

Walikuwa watoto watatu wawili wa kiume na mmoja wa kike, wa kiume mmoja alikuwa mfanya biashara mkubwa wa madini ambaye pamoja na elimu yake aliyoipata Marekani aliamua kujikita kwenye biashara ya madini na kuweza kumiliki migodi miwili.  Biashara ile ilimuingizia pesa sana na kumnfanya kuwa  mtu maarufu wenye kutikisa jiji la Arusha.

Wa pili yeye ni katibu mkuu ofisi ya Rais ambaye na yeye alikuwa na maisha mazuri, alikuwa na majumba na magari ya kifahari na wa mwisho alikuwa msichana  ambaye yeye alibahatika kupata kazi katika shirika moja la utangazaji nchini Canada.

Baada ya kukubaliana wote walipanga siku ya kukutana jiji Arusha tayari kwenda jiji Dar kwa mama yao bila kumjulisha kwa kumshtukiza. Kwa Upande wa Edna  alikuwa na furaha isiyo na kifani kukutana na ndugu zake kwa mama yao na kuweza kuwaeleza kupata kwake mchumba.
Aliomba siku ile ifike upesi ili wamfanyie mama yao surprise ya ajabu kwa watoto wake kukutana kwa pamoja asubuhi baada kufungua mlango awakute mlangoni.

************************* ********************** ***********

Mipango ya ndugu watatu ilikwenda kama walivyotaka na siku ilipotimu walikutana wote jiji Arusha kwa mkubwa wao Moses. Kila mmoja walifurahia kumuona ndugu yake walikuwa wakipenda kwa kujifananisha na Masii eti wamezaliwa bila baba.

"Jamani kaka Mose shavu dodo."
"Mbona humsemi Martin."
"Yeye sitii neno kwa jivi yupo kwenye mihela."
"Hata wewe mdogo wetu Canada imekukubali,"

“Basi wote tumshukuru Mungu kutupa afya bora.”
“Lakini kaka zangu fanyeni mazoezi kidogo mwili huo una madhara.”
“Tumekuelewa.”
“Jamani safari yetu kesho alfajiri nimeisha kodi ndege.”
“Yaani sijui mama yetu atafurahije kutoana wanaye watatu tena alfajiri kabla ya kuamka.”
“Litakuwa bonge la surprise.”
“Natamani kesho ifike upesi tukanyonye kwa mama.”
Siku ile walikesha sebuleni wakizungumza mambo mengi, alfajiri iliwakuta sebuleni. Alfajiri ilipofika walielekea uwanja wa ndege na kuondoka na ndege ya kukodi. Waliwasili jijini Dar majira ya saa kumi na mbili asubuhi.
Baada ya kuteremka kwenye ndege walikodi gari na kwenda moja kwa moja hadi Mbezi walipomjengea kwa mama yao. Walisimamisha gari mbele ya lango, kwa vile hawakutaka kumshtua mama yao, waliingia waliteremka kwenye gari na kwenda kugonga geti ambalo lilifunguliwa na mlinzi.
Alipowaona alitaka kupiga kelele za furaha walimzuia kwani hawakutaka mama yao ajue kitu mpaka atakapofungua mlango na kuwaona wanaye watatu wamesimama mbele yake. Baada ya kuingia ndani walikwenda moja kwa moja mlangoni.
Mlango wa nyumba kubwa ulikuwa umefungwa kuonesha ndani bado wamelala. Walipofika kwenye mlango walibonyeza kengere zaidi ya mara tatu. Baada ya muda walisikia sauti ya mtu kutembea. Wote walikaa mkao wa kusema kwa sauti neno la Surprise mamaaa.
Mara mlango ulifunguliwa wakati wanajiandaa kusema surprise mama, walishangaa kumuona aliyefungua ni msichana wao wa kazi. Alipotaka kupayuka kwa furaha baada ya kuwaona, walimuonyesha ishara ya kidole mdomoni kuwa asipige kelele na yeye alifanya kama alivyoagizwa,
"Vipi mama amelala?" aliuliza Edna.
"Mama?” Ajabu Eliza msichana wa kazi badala ya kujibu na yeye akauliza swali.
“Eliza kwani nimekuuliza nani?”
"Ha..ha..yupo.”
“Hayupo! Amesafiri?"
"Ha..ha..pana.”
“Hapana! Sasa yupo wapi?”
“Jana alitoka hajarudi," Eliza alijibu huku akitafuna vidole kitu kilichowashtua na kutaka kujua kuna nini.
"Hajarudi? amekwenda wapi"
"Kwa kweli sijui aliniaga tu anatoka."
"Jamani maswali huku tumesimama sio mazuri tuingie ndani," Moses alishauri.
Kabla hawajaingia ndani msichana wa kazi aliponyanyua macho baada ya kusikia geti likifunguliwa alipiga ukelele.
"Ha!"
Kauli ile ya mshangao iliwafanya wote waligeuka nyuma na kukutana na sura ya mama yao akiwa kwenye hali ya umajeruhi. Kila mmoja alitaharuki mama yao alikuwa na bandeji kubwa kichwani na mkononi na mdomo ulikuwa umevimba.
Kilichowashangaza zaidi kilikuwa mavazi ya ajabu ya nusu uchi aliyokuwa amevaa manma yao. Yalikuwa ya aibu kila mtoto wa kiume aliangalia pembeni ili mama yao aingie ndani kwanza ili ajistiri mwili wake.
Edna alijikuta akibubujikwa na machozi kutokana na hali aliyokuwa nayo mama yake, hakujari mavazi yake zaidi ya majeraha aliyokuwa nayo. Wakati huo mama yao alikuwa amepigwa na butwaa kwa kuumbuka mbele ya wanaye na kujisemea moyoni "Mungu wa ajabu."
Baada ya kuingiza ndani na kubadili nguo kwa kuvaa nguo za heshima zilizoufichwa mwili wake. Edna aliwaita kaka zake wakati huo mama yao ambaye hakutegemea kuwakuta wanaye maeneo yale

kibaya zaidi wote watatu. Mama alijikuta akiangua kilio huku kujiuliza atawambia nini wanaye kwa hali ile waliyomuona nayo kuwa anatoka wapi
Edna alimfuata mama yake huku akibubujikwa na machozi.
“Mama umeumia sana.”
Mama yake hakusema kitu aliendelea kulia akiwa amejiinamia.
“Mama kama umeumia sana twende hospitali, kina kaka tumpelekeni mama hospitali.”
“Kachukue funguo za gari yumuwahishe hospitali.”
“Wanangu siimwi mnavyofikiria.”
“Sasa mama unalia nini?”
“Wanangu nimeumbuka mchana kweupe.”
"Mama umepatwa na nini?" mama yao hakujibu kitu zaidi ya kuangalia chini huku machozi yakiendelea kumtoka.
"Mama au unasikia maumivu makali?"
Ilikuwa kitu tofauti na jinsi walivyomzoea mama yao kwa ucheshi na uchangamfu hasa anapokutana na wanaye. Walitegemea angefurahi kuwaona wanaye lakini imekuwa tofauti na walivyo fikiria zaidi ya kuona kilio cha mama yao ambacho toka wazaliwe hawajawahi kukiona.
Wote watatu walijikuta wakianza kulia, lakini Edna yeye ndiye aliyelia kwa sauti ya juu akiwa amepiga magoti mbele ya mama yake.
"Mama tatizo nini? Mbona unatuacha njia pana mama ni bahati gani kuwaona wanao wote. Tueleze umepatwa na nini ili tujue tukusaidieje. Mama umepatwa na nini mama yetu?"
Mama yao huku akilia alimpapasa mwanaye mgongoni kwa mkono mzima na kusema kwa sauti ya kilio.
"Wanangu silii kwa maumivu bali kwa majuto, Mungu kaniumbua."
"Majuto ya nini tena mama? Mungu kakuumbua nini?"
"Si waongo waliosema siku ya kwenda uchi ndiyo siku ya kukutana na mkweo."
"Mama mbona hatukuelewi?"
"Kilichopo mbele yangu najua ni mipango ya Mungu ili kuniumbua mama yenu."
"Mama bado hatujakuelewa akuumbue kwa lipi?"
"Ilikuwa siri ambayo ndiyo iliyobeba maisha yenu kwa ujumla."
"Ni siri! Iliyobeba maisha yetu. Ni siri gani hiyo mama?"
"Ni siri chafu ambayo hamkupaswa kuijua, nina imani Mungu kayafanya haya ili kuniumbua sina budi kuiweka bayana ili munielewe mama yenu najua kama nitakaa kimya nitawatesa wanangu mpaka mnakufa."
Watoto wake wote walitazamana kisha kila mmoja alirudisha macho kwa mama yake na kuendelea kumsikiliza kutaka kujua mama yao ana siri gani. Pia kutaka kujua ile hali aliyonayo mama yao imetokana na nini?
Mama yao akiwa bado ameinama alinyanyua macho na kuwatazama wanaye kila mmoja kisha alijitengeneza vizuri kitini na kusema:
"Hili nitalo liongea sikupaswa kuliongea mbele yenu ni aibu, lakini ndilo lililobeba siri ya maisha yenu. Leo mtajua mama yenu nimetoka wapi na nipo wapi na nilitaka kwenda wapi," mama alimeza mate kisha aliendelea kuongea.
"Kwanza kabla ya yote ningependa kuomba msamaha kwa lolote litakalo wakwaza kwa namna moja au nyingine kwa haya nitakayo yatamka mbele yenu."
"Kwetu sisi mama yetu huna kosa lolote litakalo tukwaza tunakupenda na kukuheshimu na hakuna chenye thamani chini ya jua kama wewe mama yetu kipenzi. Mapenzi yako hayatapungua mioyoni mwetu, bali udhuniko lako ni kilio kikubwa mioyoni mwetu, hebu tuweke wazi mama yetu mioyo yetu ipo taabuni kufikiri tusilolijua," Martin kaka yao alifikisha ujumbe kwa niaba ya wadogo zake wote waliokuwa kimya wakiwa na shauku na kilichokuwa mbale yao.
Mama yao baada ya kusikia kauli ya wanaye alifuta machozi kwa upande wa kitenge aliokuwa

amejifunika na kuzungumza kwa sauti ya chini lakini yenye kusikika.

"Kwanza wanangu naomba radhi nipo chini ya miguu yenu kwa hali mlionikuta nayo, ambayo ndiyo iliyoweka wazi tabia yangu ambayo si rahisi kwa ninyi kuijua. Hili mlililoliona ndilo lililobeta maisha yangu ambayo nilishindwa kuyabadilisha japokuwa nilikuwa na maisha mazuri.

“ Mwanzo nilifanya kama sehemu ya kujipatia kipato lakini sasa imeisha kuwa mazoea. Sawa na mvuta sigara hawezi kulala bila kupata angalau mkupuo mmoja na mimi mama yenu hivyohivyo."

"Ni nini hicho, hebu mama kiweke wazi kwa vile umeamua kutueleza." Moses ambaye muda mwingi alikuwa kimya alimueleza mama yake.

Mama yao akiwa mwingi wa aibu waliwatazama watoto wake kwa zamu kwa mara nyingine kisha alisema:

"Wanangu naweza sema maisha yangu mpaka kufikia hapa nimepitia mambo mengi mchafu na magumu ambayo ukimuhadithia mtu ataona ni uongo," alivuta pumzi huku alitengeneza vizuri ushungi wake uliokuwa umemteremka.

"Basi wanangu maisha haya ingekuwa yanaonekana jinsi mwanadamu anavyo ishi unaweza kumuonea huruma au kumdharau kama si kumchukia kabisa.

"Wanangu mnaweza kuona leo mama yenu naishi maisha mazuri hakuna nilichokikosa maishani kwa sasa, mmenijengea nyumba nzuri gari zuri na kunipatia mahitaji yote muhimu. Ni kweli, lakini historia nzima ya maisha yangu inanihukumu.

“Sikupenda wanangu mjue maisha yenu yamepitia wapi mpaka leo mpo kwenye hali hii. wanangu sikupenda lakini leo sina jinsi bila hivyo hali mlionikuta nayo hamtanielewa kama nitawaeleza nusu nusu. Historia yangu mimi mama yenu inaanzia miaka therasini na tatu iliyopita kabla sijayajua maisha ni nini.

MIAKA THELATHINI NA TATU ILIYOPITA

Nikiwa ni mtoto wa tatu katika familia ya watoto wanne wa kiume watatu na wa kike mmoja, ambaye ndiye ni mimi mama yenu niliyekuwa kiziwanda. Kwa kweli baba yangu alikuwa akinipenda sana hasa tukizingatia ni mimi pekee ni mtoto wa kike na mama yangu hakuwa na uwezo wa kuzaa tena.

Nilipewa upendeleo ambao hata kaka zangu uliwaudhi, lakini hakuna kilicho mbadilisha baba na mama yangu. Nilipofika hatua ya kwenda shule, nilitafutiwa shule ya kimataifa tofauti na kaka zangu ambao wao japokuwa walisoma za kulipia, lakini hazikuwa hazikuwa na gharama kubwa kama yangu.

Kitu kingine kilichofanya wazazi wangu wasijutie uamuzi wao wa kunipeleka shule ya gharamani akili zangu. Nilifanya vizuri katika masomo yangu na kushika nafasi za juu shuleni. Baba aliniahidi nikimaliza kidato cha sita atanipeleka Marekani kusoma.

Kama mjuavyo nilijikuta nabweteka na mapenzi ya wazazi wangu na kujua sitachukuliwa hatua yoyote kwa lolote nitalo lifanya. Nikiwa kidato cha tano ambapo nilisomea Uganda, chuoni nilikutana na kijana mmoja ambaye ni Mtanzania mwenzangu,ambaye alinivuta kwenye mambo ya mapenzi.

Nilijikuta nafanya starehe kwa fujo bila kuogopa kitendo kile kitawaudhi wazazi wangu. Wakati huo yule kijana ambaye alikuwa mwaka wa mwisho, katika uhusiano wetu ya mapenzi kwa bahati mbaya nilishika ujauzito.

Nilifikiria kuutoa lakini nilihofia kwa kuambiwa kuwa pale shuleni kuna wasichana wawili walikufa kwa ajiri ya kutoa mimba. Habari zile zilinishtua sana na kunifanya niogope kutoa kwa kuhofia maisha yangu.

Katika uchunguzi wa afya za wanafunzi niligundulika mjamzito na kurudishwa nyumbani. Wakati huo bwana aliyenipa ujauzito alikuwa ameishaondoka na kurudi Tanzania. Sikuwa na jinsi zaidi ya kurudi nyumbani Arusha ambako ndipo nilipozaliwa.

Nilipofika nyumbani baba hakuwepo alikuwa amesafiri, nilimkuta mama ambaye alishangaa kuniona muda ule. Kwa kuwa nilikuwa na uhakika wa kupendwa na wazazi wangu, sikuhofia chochote nilimweleza yote.

Mmh! Kauli ile ilimshtua sana mama na kuniomba bora tuitoe ile mimba kabla baba hajarudi. Nilimkatalia kwa kuhofua maisha yangu.

"Mama mimba inaweza kuondoka na maisha yangu!"
"Hapana mwanangu hii ndiyo njia pekee ya kukuponya kwa baba yako."
"Mama baba ananipenda hawezi kufanya lolote."
"Mwanagu humjui baba yako, mimi namjua vizuri hawezi kukubaliana na hili japo anakupenda sana."
"Wasiwasi wako tumsubiri uone."
"Hapana baba yako alimfukuza mdogo wake ambaye alikuwa akimpenda tena alikabidhiwa na wazazi wake amtunze na kumsomesha. Na yeye alifanya upuuzi kama wako baba yako alipojua mapenzi yote yaliisha na kumfukuza kama mbwa na hakutaka kumuona mpaka leo hii tunayoongea anasema hataki kumuona"
"Mama yule alikuwa ni mdogo wake lakini mimi ni mwanaye," bado nilikuwa mbishi.
"Mwanangu usiwe mbishi heri nusu shari kuliko shari kamili," mama aliendelea kunibembeleza.

Sikuwa na jinsi zaidi ya kukubaliana na mama kwenda kuitoa mimba kabla baba hajarudi ikiwezekana awahi kunirudisha shuleni. Mama alinipeleka hadi kwa daktari mmoja maarufu sana jiji Arusha. Baada ya kukutana na Daktari alikubaliana na mama gharama za kunitoa ujauzito. Mama alilipa na kupelekwa chumba cha kutolea mimba, niliingizwa chumba cha kutolea mimba. Nilifanyiwa vipimo kabla ya kunitoa, lakini mambo yalikuwa kinyume.

Ujauzito wangu ulikuwa umekaa vibaya ambao usingiweza kutoka kama wangeutoa, ungetoka na roho yangu. Hapo mama alichanganyikiwa na kushindwa kujua atatumia njia gani kuificha siri ile. Hakuamini kauli ya Daktari yule tulikwenda hospitali zaidi ya nne jibu lilikuwa lile ile, kuwa mimba haiwezi kutoka.

Mama hakuwa na jinsi zaidi ya kukubali matokeo na kuamua kumsubiri baba na yeye ana uamuzi gani? Japokuwa mama alionekana mwenye wasiwasi kwa upande wangu sikuwa na hofu yoyote kwa baba hasa nikizingania mapenzi yake kwangu yalikuwa makubwa sana.

Baada ya siku tatu baba alirudi kutoka safari zake za nje ya nchi, tulimpokea kwa furaha na bashasha. Aliponiona alishtuka kuniona nipo nyumbani siku za shule. Mama alimtuliza kwa kumwambia
"Poa kwanza, hata ujatulia na safari."
"Mke wangu nitulie kwa uchovu gani, hasa kwenye tatizo wakati mwenetu alikuwa shule leo yupo nyumbani tena siku za shule kama anaumwa atibiwe awahi shule na kama kuna tatizo lingine litatuliwe haraka huu si muda wa kucheza na elimu."
"Si umefika utayasikia haraka ya nini kuna mtu anaondoka," mama alizidi kumtuliza baba.

Kauli ile ilimfanya baba anyamaze na kuendelea na mambo mengine. Japokuwa nilikuwa na uhakika baba awezi kufanya lolote kutokana na kisanga changu, lakini hofu kidogo ilinitawala kutokana na maneno yake juu ya kucheza na elimu.

Nikiwa nimejilaza chumbani kwangu baada ya chakula cha usiku, nilisikia mlango ukigongwa kwa nguvu kama ameingia askari. Nilinyanyuka na kwenda kufungua mlango. Baada ya kufungua, mlango ulifunguliwa kwa nguvu kitu kilichonitisha.

SURPRISE YA AIBU - 02

Baba kwa hasira alinifokea kwa sauti ya juu kitu ambacho hakuwahikukifanya toka nizaliwe. Mara nyingi mama aliponifokea baba ndiye aliye kuwa mtetezi wangu. Kwa hali ile hofu ilinijaa moyoni, kwa hasira baba aliniuliza huku akiwa ameshikilia ile barua niliyopewa shuleni.
"We Moureen hiki ni nini?" alisema huku akinitupia ile kalatasi.
"Bahati mbaya baba," nilijibu huku nikiwa nimepoteza ujasiri na kuanza kutetemeka.
"Mmh! Bahati mbaya eeeh," aliongea kwa sauti ya chini.
"Ndi.ndi.yoo...ba.aba."
"Bahati mbaya," aliongea kwa sauti ya juu ikifuatiwa na kofi zito lililotua kwenye shavu la kushoto na kunirusha kwa nyuma mpaka chini, haja ndogo ilinitoka bila kupenda. Nikajua siku hiyo patakuwa hapatoshi. Niliikumbuka hofu ya mama juu ya hali atakayokuwa nayo baba baada ya kusikia ujinga wangu.
"Wewe nguruwe nasema hivi kuanzia sasa hivi nenda kwa nguruwe mwenzio aliyekubebesha uchafu huo."
Mmh! niliona mambo mazito, nilipiga magoti mbele ya baba kuomba msamaha.
"Baba naomba unisamehe."
"Nikusamehe kwa lipi?"
"Kwa hii hali niliyokuwa nayo."
"Sikiliza mwanangu kwa vile umekuwa mtu mzima, sina budi kukuruhusu ukaishi na umpendaye kwa vile kuwa kwenu unaona unachelewa."
"Baba simjui anapoishi."
"Atii nini?" kauli yangu ilimuudhi baba.
"Ni kweli baba ni bahati mbaya ilikuwa kama ajali, tena alinibaka mi nilikuwa sitaki," nilijaribu kujitetea.
"Nasema hivi naomba uondoke machoni kwangu, usiku huu na tusionane mpaka mauti yatakapo tuchukua."
Ilikuwa kauli nzito ambayo sikuitegemea kuisikia toka kinywani kwa baba yangu kipenzi. Siku hiyo nililia sana, mama alinisaidia kumuomba msamaha lakini hakuwa tayari kunisamehe hata yeye alitishiwa kufukuzwa kama ataendelea kuninitetea.
Kwa mara ya kwanza mapenzi ya baba yangu yaliyeyuka kama donge la mafuta kwenye kikaango cha moto. Baba alikuwa mbogo alinifukuza usiku ule. Sikuwa na jinsi nilikwenda kwa rafiki yangu ambaye alikuwa amepangiwa chumba na rafiki yake wa kiume. Alinipokea na kunipa hifadhi ya kulala mpaka siku ya pili.
Asubuhi shoga yangu alinieleza:
“Moureen zile ni hasira za baba yako lakini leo ukirudi atakusamehe.”
“Mmh! Siamini kama baba atabadirika.”
“Inawezekana hata yeye anajilaumu kukufukuza pengine usiku alikutafuta.”
“Eti eeh!”
“Shoga rudi kwani baba yako anajua utaishi vipi?”
Nilijifikiria na kukubaliana na shoga yangu kurudi siku ile kuomba msamaha. Niliamini kabisa alichozungumza baba yangu ilikuwa ni hasira za ghafla, lakini nikirudi kumuomba msamaha atanisamehe kwa kujua mimi ndiye mtoto wake sina pa kwenda.
Nilikubaliana na wazo la rafiki yangu baada ya kupata kifungua kinywa ambacho kilinishinda, niliamua kurudi nyumbani kuomba msamaha.
Niliwasili nyumbani na kubahatika kuwakuta wazazi wangu wote wawili waliokuwa wamekaa sebuleni wakijadili jambo. Mama alikuwa wa kwanza kuniona, alinikaribisha.
"Karibu mwanangu," kauli ile ilimfanya baba ageuke kuangalia nani aliye karibishwa. Aliponiona

mimi kwa sauti ya juu yenye kila aina ya ghadhabu alisema:
"We shetani mwanamke umefuata nini?"
"Baba Moureen msamehe mtoto," mama aliniombea msamaha kwa baba
"Nimsamehe eeh, subiri uone nitakavyo msamehe," baba alisema yale huku akisimama na kuelekea chumbani.
Nikiwa bado nimesimama karibu kabisa na mlango wa kuingilia sebuleni. Nilishtushwa na sauti ya mama:
"Moureen mwanangu kimbiaaaa," nilipotupa macho baba alikuwa na bunduki mkononi, lakini mama kwa ujasiri mkubwa alifanikiwa kumdaka na kuanguka naye chini. Wakati huo mama alikuwa akiendelea kupiga kelele.
"Moureen mwanangu kimbia baba yako atakuua."
Baba naye alijitahidi kunyanyuka lakini mama alikuwa amemshikilia madhubuti.
"Niache mama Moureen nimuulie mbali shetani huyu bora nikanyongwe kuliko aibu hii," nilijikuta nimeshindwa nifanye nini miguu ilinitetemeka.
"Moureeeen kumbiaaaa," mama alizidi kusisitiza.
Wakati huo baba alikuwa ameamka bunduki akiwa amedondoka mbali, muda wote nilikua bado nimepigwa butwaa. Baba aliponyanyukaili aiwahi bunduki hapo ndipo nilipojua kilichokuwa mbele yangu si maigizo bali kweli nilitimua mbio huku nyuma nilimsikia baba akifoka kwa hasira:
"Bahati yako ningekufumua kichwa mwana haramu mkubwa."
Nilikimbia bila kuangalia nyuma mpaka kwa shoga yangu nilikuta mlango upo wazi niliingia ndani bila kupiga hodi nilipofika tu nilianguka chini na kupoteza fahamu.
Rafiki yangu alinipatia huduma ya kwanza, kisha alitaka kujua yaliyojili nilipokwenda, Nilimweleza yote.
"Utani huo Moureen!" shoga yangu alishangaa.
"Bila mama leo ningekuwa marehemu."
"Mmh! Kama imefikia hivyo kuna umuhimu kumtafuta baba mwenye mimba hii hakuna njia nyingine kwa hatua hiyo sidhani kuna suruhu," shoga yangu alinishauri.
Rafiki yangu aliniombea nauli ya kuja Dar kwa mpenzi wake ambaye alinipa na pesa za matumizi. Kesho yake nilifunga safari hadi Dar, jiji ambalo toka nizaliwe nililiona kwenye Luninga tu. Nilikumbuka aliniambia Dar anakaa Mikocheni nyuma ya jengo la super market Shorpers Plaza.
Alinieleza nikivuka bar moja wanayouza kiti moto nihesabu nyumba mbili kuna mtaa unaingia kulia, mbele kuna muuza chipsi nikate kushoto na kuifuata njia ya moja kwa moja kuna fundi viatu nyumba hiyo ndiyo anayoishi.
Niliwasiri Dar majira ya saa tisa alisiri na kukodi gari hadi Mikocheni. Nilimuomba aniteremshe pale Shorpers Plaza ili nisiipoteze ramani yangu, niliteremshwa Shopers Plaza na kuangalia ramani yangu haikuwa tofauti na maelezo aliyonipa.
Niliiifuata njia aliyonielekeza, muda ule ulikuwa ni saa kumi na moja kasoro. Kuchelewa kote kilitokana na fureni kubwa ya magari ambayo ilikuwa ni ajabu kwa sisi watu wa mikoani kwenye uchache wa magari.
Nilifanikiwa kufika kwenye ile Bar ambayo kweli niliona kiti moto kikiuzwa. Nilihesabu nyumba mbili na kutokea kwenye njia iliyoingia kulia, mbele nilikutana na banda la chipsi .Nilikata kushoto, huwezi amini japo kuna mitaa na vichochoro ramani ilikuwa haipotezi wala haina haja ya kumuliza mtu.
Nilifuata kijinjia kidogo hadi mbele ambapo nilimkuta mshona viatu. Nilipo muona kwanza nilishusha pumzi na kumshukuru Mungu kwa kufika bila kupotea.Nilisabahi yule kaka
"Za saizi kaka."
"Nzuri karibu."
"Asante, shikamoo."
"Marahaba."

"Sijui kaka hapa ndipo anapokaa Shauri Kati au Shaka Zuru?"
"Wewe ni nani?" yule mkaka aliniuliza huku akinitazama nilivyo.
"Mmh! Mimi ni rafiki yake tulikuwa tunasoma pamoja Uganda."
"Ooh! Umefika, ndio hapa."
"Yupo?"
"Kwa sasa hayupo hapa amehama."
"Mungu wangu! Amehamia wapi?" nilishtuka.
"Usihofu na karibu tu."
"Ooh! Afadhari nilishtuka."

Yule kaka alimuachia mtu kazi yake na kunipeleka anapoishi Shauri, hapakuwa mbali kama nyumba ya sita kutoka kwao. Tulipofika aligonga mlango, mlango ulifunguliwa na Shauri alitoka aliwa kifua wazi amevalia bukta kwa chini.

Aliponiona alishtuka na kusema:
"Aah! Moureen!"
"Ni mimi Shaka," nilijikuta nikitabasamu kumuona kipenzi changu Shaka.
"Karibu sana."
"Asante," nilijibu huku nikiingia ndani, kumbe Shaka alikua Artisit Mchoraji. Kumbe muda ule alikuwa akichora. Baada ya kukaa na kuniagizia soda alitaka kujua mbona nipo pale wakati wenzangu wanaendelea na masomo.
“Moureen mbona huku kipindi cha masomo?”
Nilimueleza nia na madhumuni ya kuniona mbele yake, nilimuona akishtuka na kuuliza.
"Moureen utani huo!"
"Kweli kabisa na sina pa kukimbilia."
"Moureen tafuta mwingine wa kumbambikia mimba hiyo sio mimi?" He! Shaka naye aliniruka.
"Shaka hii mimba mwenyewe ni wewe, naomba unipokee nitakuwa mgeni wa nani na wewe ukinikataa," nilijikuta nikichanganyikiwa mtoto wa kike.
"Moureen naomba unielewe sina msaada mwingine zaidi ya kukupa hifadhi ya leo, kesho nakupa nauli urudi kwenu."

Ngoma ilikuwa nzito Shaka naye alinitolea nje, niliona dunia imenigeuka hata mwenye mzigo kanikataa.Nilipojaribu kumlazimisha niliambulia kipigo, mmh nikaona hakuna haja ya kulazimisha maisha mjinga mimi. Wazo la kujiua nililikataa na kuwa tayari kupambana na maisha.

Siku ya pili hapakuwa na mabadiliko yoyote zaidi ya kupewa nauli ya kurudi Arusha. Nilijiuliza Arusha nitarudi kwa nani, niliamua kubaki Dar liwalo na liwe. Hapo ndipo nilipo ingia kwenye ukahaba nikiwa na ujauzito wangu kwa kulala ovyo.”

Kauli ile iliwafanya watoto wake kutokwa na machozi, lakini mama yao aliendelea na mkasa mzito wa kusikitisha.

“Basi katika zungukazunguka yangu nilipata shoga ambaye alinikaribisha kwake, tukawa wote usiku tunatoka kutafuta wanaume. Mungu hamtupi mja wake nilijikuta nayaendesha maisha yangu bila matatizo.

Muda ulipofika ndipo nilipo jifungua mtoto wangu wa kwanza ambaye ni wewe Martin. Nilimlea mwanangu kwa kazi yangu ya ukahaba, Mwanangu kwa kweli alikuwa kwenye mazingira magumu kwa kumuacha peke yake chumbani na mimi mama yake kwenda kwenye ukahaba.

Mungu naye alimjalia alikuwa bila tatizo lolote kama maradhi ni sehemu ya maisha ya mwanadamu.Ile kazi ilinisaidia kuweza kupanga chumba changu na kuweza kuwa na vitu vyote muhimu chumbani kwangu. Aliyeingia chumbani kwangu alijua ni mfanya biashara mwenye pesa.

Sikuchukua muda mrefu mwanangu Martin alipofikisha umri wa mwaka mmoja na nusu, nilishika ujauzito mwingine. Kwa kweli sikujua ile mimba ni ya nani kwa kuwa nilikuwa nakutana na wanaume wengi wengine wabishi kutumia Kondomu. Kwa vile nilihitaji pesa yao sina budi kukubaliana nao.

Niilea ile mimba ambayo baba yake sikumjua mpaka nilipofanikiwa kujifungua salama mtoto wa pili

ambaye ni wewe Moses.
Wakati huo kidogo pesa nilikuwa nazo. Mwanangu alipata huduma nzuri kwa kuwa na mhudumu ambaye alimhudumia mimi nikiwa sipo.
Niliendelea na kazi yangu ya ukahaba ambayo iliendeleza kupunguza makali ya maisha. Siku moja nikiwa katika mawindo yangu nilichukuliwa na wazungu. Siku zote kazi yetu tulipenda tukutane na wazungu ambao dau lao lilikuwa kubwa tofauti na waswahili hawaschelewi kukukopa.
Lakini siku hiyo haikuwa kama nilivyo fikiria, waliniuliza kwa wote ni shilingi ngapi. Walikuwa wanne, niliwajibu kwa wote watanipa dola mia nne. Walikubali na kunipa zote taslimu ambazo nilimuachia shoga yangu kwa kuhofia kuzurumiwa.
Niliingia kwenye gari na kuondoka nao kuelekea nisipo pajua, siku zote kazi zetu tulimwachia Mungu kulinda maisha yetu. Nilipofika kwao kumbe haikuwa hivyo walikuwa wamepanga kunifanyisha mapenzi na mbwa wao wawili kwa nguvu.
Nilipokataa walinilazimisha kwa kunitishia na bastora, hata hivyo sikuwa tayari walinipiga na kunifunga kamba kisha waliwachukua mbwa wao na kuniingilia kimwili huku nikisikia maumivu makali. Siku hiyo nilijuta kufanya ukahaba kwa kuingiliwa kinyume na maumbile na wanyama wale.
Mpaka wananiachia nilikuwa hoi sijiwezi, walinichukua na kwenda kunitupa kwenye mtaro. Niliokotwa na watu nikiwa sina kktu mwilini, walinichukua na kunipeleka hospitali.
Nilipata fahamu ziku ya pili jioni wakati huo nilikuwa nimeishapatiwa matibabu ya hali ya juu ikiwa pamoja kupigwa bomba. Kabla ya kutoka polisi walifika kuchukua maelezo. Kwa vile sikuwajua vizuri ila nilikuwa nawafahamu nilitoa maelezo nao waliahidi kuwasaka mpaka kuwatia nguvuni.
Baada ya wiki mbili walifanikiwa kuwakamata baada ya kutega mtego seheme yenye tunayofanya biashara ya miili. Kitu cha ajabu baada ya kukamatwa wale Wazungu waliandika maelezo na kuwekwa ndani kisha nikaelezwa nirudi siku ya pili.
Nilikwenda nyumbani na siku ya pili nilirudi polisi nikiwa na ushahidi wa shoga zangu waliokuwepo siku nilipochukuliwa. Kila kitu kilikuwepo ikiwemo taarifa ya daktari vilionesha kweli niliingiliwa na mbwa, kilichotakiwa kuwafikisha mahakamani na kufunguliwa mashtaka
Usitaajabu ya Musa utayaona ya Filauni, siku ile nilipofika kibao kikanigeukia mimi eti kumbe wale Wazungu walikuwa na RB yangu alikuwa nayo aliyofungua muda mrefu ya kuwaibia dola laki moja na walikuwa wakinitafuta. Basi wanangu mimi ndiye niliye ingizwa hatiani na kufikishwa mahakamani mara moja na kufungwa mwaka mmoja baada ya kujitetea nina watoto wadogo. Hebu wanangu ona jinsi uonevu ulivyo fanywa juu yangu kwa vile nilikuwa mnyonge sina kitu.
Nilikubali matokea lakini moyoni nilijiapiza nitakapotoka kila aliyehusika hastahili kuishi duniani. Basi sikuwa na jinsi nilitumikia mwaka gerezani.
Nilipotoka nilianza msako wa kuwasaka wabaya wangu, wanangu nilimuua mmoja mmoja kila kukicha. Kwa wale wazungu niliua mpaka mlinzi na mbwa wao. Nilipomaliza kumuua mkuu wa polisi aliyeshiriki kubadilisha kesi yangu ndipo nilipotorokea Mwanza.
“Uliwauaje wote hao bila kushikwa?” Edna alijikaza na kumuuliza mama yake.
“Mnajua wale wazungu walikuwa ma x-part waliokuwa wakisimamia miradi mingi nchini na walikuwa wakilindwa na serikali. Kesi kama ile haikuwa kwangu tu kumbe mchezo ule tulifanyiwa wanawake wengi waliokuwa wakifanya biashara kama yangu.
Ilionesha mkuu wa polisi niliyemuua alikuwa akihongwa na kuwageuzia makosa wote waliokwenda kushtaki na kuwafanya wasichana wengi wakitendewa unyama kukaa kimya.
Baada ya kutoka gerezani nikiwa na hasira na wote walionitenda kuanzia mkuu wa polisi hakimu na hao wazungu ambao waliendelea na tabia za kutudhalilisha wanawake.”
“Mama wakati unafungwa kina kaka walikuwa wapi?” Edna aliuliza tena kwani kaka zake walikuwa wamepigwa na bumbuwazi na kuona kama aliyokuwa akiyasema mama yao ni hadithi ya ndotoni.
“Kuna shoga yangu mmoja aliwachukua na kukaa nao, bahati nzuri nilikuwa na fedha ya kutosha katika akaunti yangu hiyo niliamini hata ningefungwa miaka miwili ingeweza kuwasaidia. Basi baada ya kurudi nilitembelea sehemu zangu kuendeleza kazi yangu ya ukahaba kuendeleza kujipatia riziki

baada ya akiba yangu kukuta imebakia kidogo kwa vile sikuwa na kazi nyingine niliamini kazi ile ndiyo mkombozi wangu.
Kwanza niliwauliza mahoga zangu kuhusu mchezo wa wale wazungu kuwafanyisha mapenzi na mbwa. Niliambiwa mzungu mmoja alifukuzwa nchini baada ya kesi kumkalia vibaya baada ya msichana mmoja kumpata mtu wa kumsimamia kwenye kesi yake na kulipwa fedha nyingi lakini na yeye kazi ya ukahaba ilikuwa kwenye damu hakuacha japo alipunguza na kuchagua wanaume wenye fedha kwani alikuwa akija kazini na gari lake.
Nilielezwa wakati narudi walikuwa wakiwachukua wanawake na kukubalia kufanya nao mapenzi wote watatu. Japokuwa wanasema ulitaka ule ushibe lakini ulikuwa ukitoka na fedha nzuri. Baada ya kuelezwa vile niliendelea kuwawinda kwa siri bila mashoga zangu kujua dhamilia yangu ni nini kwa washenzi wale nilitembea na dawa ya kulevya ya kupaka kwenye matiti ambayo huitumia kama unataka kumwibia mtu pia kisu nilichokificha kwenye mkoba wangu.
Nilifanya kazi kwa taadhari kubwa ili nisirudie kosa  la awali, sikuwa tayari kwenda na mtu mwenye gari bali kufanya mapenzi ya papo kwa papo na kumalizana.  Niliendelea na kazi yangu huku nikifanya mawindo ya watu wangu.  Sikutaka kuanza na mkuu wa polisi na hakimu kwanza kwa vile nilijua wale ni watu wa kumalizia.
Siku moja nikiwa  lindoni mwangu lilikuja gari na kushangaa kuona mashoga zangu hawalikimbilii, nilijiuliza kuna nini. Nilipouliza niliambiwa:
“Shoga leo hatutaki wale wazungu wana mchezo mbaya, leo hawapati mtu tumewaambia kama kwenda na mmoja sawa lakini wote watatu hatutaki.”
Kauli ile ilinifanya nichekelee moyoni, nilijisogeza mbele hadi kwenye lile gari waliponiona walinieleza kama nitakubali watu watatu sawa ilionesha wamenisahau.
Nilikubali kuwa nipo tayari, niliongozana hadi kwao, moyoni nilikuwa na dhamila mbaya kila nikikumbuka moyo unanitetemeke na kumuomba  Mungu anisamehe.
Tulipofika niliwaeleza nitafanya mapenzi na wote lakini kwanza na mmoja mmoja  kisha baadaye nitafanya na wote kwa pamoja. Tena niliwaeleza kwanza nitafanya mapenzi kwa kila mmoja kuwa chumbani kwake. Bila kujua nimedhamilia nini walikubali. Basi nilianza kwa kuingia kwenye chumba cha mmoja na kuondoa nguo zote nikijifanya nimepandwa maruhani ya mapenzi.
Wakati wa kuandaana nilipaka dawa yangu kwenye matiti bila kujua kisha nilimwambia anyonye ili kunipandisha mdadi, bila kujua alifanya nilivyotaka. Haikuchukua muda alinyonya kisha nilimuona akilegea na kujilaza pembeni.
Nilichukua mto na kumziba pumzi usoni, sikuutoa mpaka alipotulia nikijua nimemaliza kazi kisha nilimlaza vizuri.
Nilijipaka dawa yangu tena kwenye nyonyo  na kutoka bila kitu mwilini na kwenda chumba cha mzungu mwingine aliyekuwa akinisubiri kwa hamu sana.
Kama kawaida baada ya kupanda kitandani nilimuomba anyonye matiti na yeye alinyonya baada ya muda alilegea na kummaliza kama mwenzake.
Kumbe wakati nammalizia yule mzungu wa pili mzungu wa tatu sijui alishtukia vipi nilimuona akija huku akimwita mwenzake kwa sauti ya juu.

SUPRISE YA AIBU-03

Nilijipaka dawa yangu tena kwenye nyonyo  na kutoka bila kitu mwilini na kwenda chumba cha mzungu mwingine aliyekuwa akinisubiri kwa hamu sana.
Kama kawaida baada ya kupanda kitandani nilimuomba anyonye matiti na yeye alinyonya baada ya muda alilegea na kummaliza kama mwenzake.
 Kumbe wakati nammalizia yule mzungu wa pili mzungu wa tatu sijui alishtukia vipi nilimuona akija huku akimwita mwenzake kwa sauti ya juu.
“Mr Rich kuwamakini Mr Rich kuwa makini.”
Kwa haraka niliteremka kitandani na kujificha nyuma ya mlango, aliingia na bastora mkononi akili yake ikiwa kwa mwenzake ambaye nilikuwa nimeisha msafirisha kuzimu.  Nilijua nimekufa kwa vile sikuwa na ujanja wowote wa kujiokoa kwa mzungu yule  aliyekuwa na siraha mkono pili hata mwili wake kama angenikamata basi ningefia mkononi kwake.
Nikiwa natetemeka mpaka haja ndogo ilinitoka baada ya kuona akimpima mwenzake mapigo ya moyo. Niliona ile ndiyo nafasi yangu ya kutoka mbio, nilikurupuka nyuma ya mlango na yeye alimuacha mwenzake na kunifuata. Kwa vile nilijua mlango umefungwa nilijitahidi kuufunga ule mlango ili nimfungie ndani. Wakati huo yule mzungu alikuwa akija mbio, nilifanikiwa kuufunga ule mlango na kumfanya ajigonge mlangoni na kuanguka chini.
Alianguka kwa kishindo, nilifunga mlango kwa komeo kwa nje kisha nilichungulia ndani na kumuona amelala chini damu zikimtoka kichwani. Nilikwenda mpaka jikoni na kufanikiwa kupata kisu kikubwa ambacho nilirudi nacho na kuufungua mlango wakati huo roho ya damu ilinijaa.
Nilimfuata chini alipolala huku nikiwa na hasira niliteremsha mapigo mfurulizo ya kifuani mpaka alipotulia.  Nilinyanyuka na kujifuta damu kisha nilivaa nguo zangu. Nilianza kupekua kila kona na kufanikiwa kupata dola laki nne, nilizifunga vizuri kisha nilichukua bastora hadi kwenye banda la mbwa na kuwaua mbwa wote na kwenda kwenye moja la gari lao na kutoka nalo.
Mlinzi alipoangalia ndani ya gari na kuniona mimi alishtuka na kunihoji:
“Vipi mbona unatoka na gari?”
“Siyo juu yako fungua geti,” nilimjibu kwa sauti ya ukali.
“Kazi yangu ni ulinzi nina haki ya kuuliza,” mlinzi naye alikuwa mbishi.
“Sikiliza we kidampa hebu fungua geti kabla sijakupoteza!” nilimtisha afungue mlango.
“Siwezi mpaka nipate ruhusa ya mabosi wangu.”
Niliona kama ananichelesha nilichukua bastora iliyokuwa pembeni yangu na kumshuti. Niliteremka haraka na kwenda kufungua geti kisha nilirudi kwenye gari na kuliondoa kwa kasi.
Nilitembea huku moyo wangu ukiwa na hasira ya kunywa damu ya mtu.Nilikwenda na gari hadi mjini ambako nililiacha njiani na kuchukua teksi iliyonipeleka nyumbani. Kwa wasiwasi wa kukamatwa sikutoka ndani kwa siku tatu huku nikisikiliza  taarifa kwenye vyombo vya habari ambavyo vililipoti vifo vya wazungu watatu  na mlinzi wao waliouawa kinyama na mtu asiyejulikana.
Nilitulia kwa muda wa mwezi mzima nikiwa mtu wa kujificha ikiwemo kuhama nilipokuwa nakaa na kuhamia nje ya mji. Baada ya hali kutulia nilianza msako wa mkuu wa polisi na hakimu. Nilifuatilia nyendo zao na kujua kila mmoja anakunywa wapi.
Pia niliona kuwapata siyo kazi kutokana na tabia zao za unywaji na kupenda wanawake. Niliona nianze na hakimu kwa kujua polisi msako wake ni mkubwa kuliko wa hakimu. Hakimu alikuwa akikaa maeneo ya Mikocheni na alikuwa akipenda kunywa kwenye baa moja maarufu iliyopo Kinondoni. Niliamua kumfuatilia nyendo zake ambazo nilizielewa, siku moja nilimkuta kwenye baa hiyo akiwa amekaa peke yake akinywa bia yake huku akichati na simu. Kwa vile nilikuwa nimevaa kiutata niliamini kila mwanaume alitamani kuwa na mimi. Nilisogelea meza yake na kumsalimia:
“Habari za saizi?”
Kabla ya kuitikia alinyanyua uso na kunitazama kisha alishusha pumzi ndefu na kusema:
“Ooh! Sorry, karibu mrembo.”

“Hapana nakusalimia,” nililegeza sauti.
“Ooh! Nzuri mrembo karibu.”
“Asante, vipi una mtu hapa?”
“Nipo peke yangu karibu mtoto mzuri.”
Nilikaa na kujifanya natoa simu kwenye mkoba na kujifanya nasoma kitu kumbe ilikuwa kumlia pozi.
“Mmh! Binti unatumia kinywaji gani? Aliniuliza baada ya uhudumu kuja kusimama mbele ya meza yetu.
“Heinken.”
“Na nini mrembo?”
“Kwanza hiyo inatosha kuanzia mi si mnywaji sana.”
Baada ya vinywaji kuletwa nilitulia na kunywa kistaarabu, kitu kilichomfanya hakimu kutaka kunijua zaidi.
“We ni mgeni?”
“Si sana.”
“Mwenyeji wa wapi?”
“Arusha.”
“Ooh! Nimefurahi kuwa na wewe nina imani leo tutakuwa pamoja.”
“Mmh! Na mkeo?” nilijifanya kulia wivu.
“Mke wangu nikirudi kwangu, sasa hivi mimi nipo na wewe mtoto mzuri.”
“Mmh! Kama hivyo basi wewe tu,” nilijifanya kulegea.
Baada ya chakula tulikubaliana kwenda nyumba ya wageni si kwa kulala kwa mapenzi ya muda mfupi kwa kisingizio nipo kwa baba yangu mdogo siruhusiwi kulala nje. Tulitoka pamoja kwenye gari lake na kuingia, nilipata wazo la haraka la kumuulia ndani ya gari ili kufuta ushahidi.
Baada ya kutoka eneo la baa niliacha gari liende mbele kidogo na kumuomba alisimamishe pembeni.
“Kuna nini sweet?”
“Nina hamu mpenzi naomba uninyonye matiti kidogo uzipunguze.”
“Vumilia nitazishusha sasa hivi.”
“Hapana ninyonye,” nilisema huku nikizitoa matiti yangu ambazo yalimbabaisha na kukubali kupaki gari pembeni na kuanza kuyanyonya matiti yangu. Japokuwa  alinipandisha mzuka lakini lengo langu lilikuwa roho yake.
Aliendelea kulinyonya kwa ufundi mkubwa sana mpaka nikajikuta namaliza haja zangu bila kupenda, lakini lengo langu kwa siku ile halikuwa hilo zaidi ya roho yake. Baada ya kunyonya kwa muda nilimuona akianza kulegea na kuliachia ziwa kisha alijilaza pembeni.
Nilimtikisa na kugundua amelegea nilichukua mto ndogo ndani ya gari na kumziba nao usoni kwa kumkandamiza kwa nguvu. Kwa vile hakuwa na nguvu hakuweza kunizuia nilimbana mpaka alipopoteza uhai nilimlaza pembeni na kuteremka zangu kwenye gari, nilifunga mlango na kuondoka zangu.
Nilitembea haraka mpaka mbele na kukodi bodaboda mpaka Magomeni ambako nilikodi teksi mpaka nyumbani. Nilitulia ndani sikilizia kwenye vyombo vya habari vitaripoti vipi kifo kile. Taarifa ya asubuhi kwenye radio zote zilielezea Hakimu Kiondo alivyokutwa amekufa kwenye gari lake.
Vyanzo vya habari vilisema alionekana ameongozana na mwanamke mmoja mrembo na kwenda kwenye gari lake na baadaye gari lake kuonekana hatua chache na baa aliyokuwa akinywa.
Polisi walisema wanamsaka mwanamke aliyetoka naye japo ilikuwa vigumu kunigundua kwa vile hakuna hata mmoja aliyekuwa akinifahamu pia alikuwa mgeni maeneo yale. Baada kufanikisha kifo cha Hakimu nilitulia kwa miezi mingine miwili kujipanga kwa ajili ya kummaliza mkuu ya kituo ambaye wakati huo alikuwa OCD katika wilaya moja mkoani Morogoro.
Mwanamke baada ya kujipanga nilifunga safari mpaka Morogoro na kupanga kwenye hoteli moja yenye hadhi mkoni Morogoro. Nilianza kumfuatilia OCD Mzizire kwa siku tatu  na kugundua bado wana tabia zilezile za kunywa kwenye baa kubwa pia kupenda watoto wazuri.

Baada ya kujua baa anayokunywa nilikwenda siku moja kwenye ile baa na kutafuta siti ya karibu na alipokuwa amekaa na wapambe wake wakinywa. Nilimwita mhudumu.
“Habari dada.”
“Nzuri, karibu.”
“Asante, samahani dada yangu.”
“Bila samahani.”
”Eti mzee Mzizire anakunywa kinywaji gani?”
“Serengeti.”
“Na wenzake?”
“Kuna anayetumia ndovu, konyagi na Tusker.”
“Kila mmoja mpe tatutatu mwambie mzee  Mzizire ofa yangu kwake.”
“Sawa.”
“Shilingi ngapi?”
“Usiwe na wasi nitakwambia baada ya kuhudumia, wewe je, huagizi?”
“Mi niletee Heinken moja.”
“Baridi, moto?”
“Moto hali ya hapa ni baridi.”
“Dada barudi ipo wapi wewe mgeni?”
“Si sana.”
Yule msichana aliondoka na kunifanya niendelee kumtazama kwa uchu mzee Mzizire, kila nilipokumbuka alivyonifanyia moyo uliniuma na sikutaka kumsamehe hata kidogo, kwa tabia zake za kuwakandamiza wanawake na kuwatetea wazungu waliowafanya vibaya wanawake kwa kuwafanyisha mapenzi na mbwa na mwisho wa siku wanafungwa wao bila kosa.
Baada ya muda nilimuona yule mhudumu akiweka tlei la vinywaji kwenye meza. Nilimuona akiuliza, mhudumu alinionesha mimi ambaye alimpokea kwa tabasamu kali. Niliwaona wote wakinishuku kwa kushika vifuani vyao nami nilijibu kwa kushika changu kuonesha nikubali.
Alipotoka pale alinileteа heinken yangu na kunifungulia na kutaka kuniwekea kwenye glasi, nilimkataza na kujiwekea mwenyewe na kupiga funda moja na kutulia. Nilifanya kuangalia chini ili niwape nafasi ya kuusanifu uzuri wangu ambao ulinifanya nijiamini muda wote.
Siku zote huwa naamini wakubwa ndiyo wanapenda kujipendelea kizuri lazima wakitake wao. Baada ya muda yule dada alikuja na bei nne na kutaka kuziweka juu ya meza yangu.
“Vipi dada?” nilimuuliza.
”Mzee amesema nikuhudumia nikupe chochote unachokitaka.”
“Mwambie asante, leo sijisikii kunywa sana, sina uhakika hata kama bia hii moja nitamaliza.”
“Dada si ungechukua hata kama hunywi ungenipa mimi mdogo wako.”
“Usiwe na wasiwasi we rudisha nitakupa elfu kumi ya matumizi unasemaje?”
“Duh! Dada yangu utaokoa maana leo hali ni mbaya.”
Nilifungua mkoba wangu na kuchukua noti ya elfu kumi na kumpa.
“Hii ya nini?”
“Yako.”
“Na bili?”
“Hujaniambia kiasi gani pia hujawaongezea bia nyingine.”
“Kwa hiyo niwaambiaje kuhusu bia hizi?”
“Mwambie kama nilivyokwambia kuwa sijisikii kunywa bia leo, labda kesho nitaungana nao.”
“Haya dada, asante sana.”
Yule mhudumu aliondoka na kuniacha nikiibembeleza bia yangu ambayo niliiweka kuzugia tu kwa siku ile sikuwa  mnywaji kabisa zaidi ya kumtamani Mr Mzizire kama Simba mwenye njaa aliyemuona Swali akinywa maji pembeni yake.
Baada ya muda yule mhudumu alinifuata na kunileteа kimemo toka kwa Mr Mzizire.

Sorry mrembo tunaweza kuwa pamoja leo?
Baada ya kukisoma nilitabasamu kumfanya aliyeleta ujumbe ambaye nilijua alikuwa akinifuatilia kujua nitaupokeaje. Tabasamu langu lilikuwa la kwanza kumpa matumaini.
Baada ya kusoma nilimuomba kalamu mhudumu na kunipa na kugeuza kalatasi kwa nyuma na kuandika.
Kwa leo au kwa siku zote?
Nilimpa mhudumu aliyempelekea baada ya kusoma naye aliandika kikalatasi kingine.
Nimekupenda sana nina imani itakuwa siku zote.
Nilipoletewa nilisoma na kumjibu.
Sawa, lakini sipendi kuchezewa na wanaume! Nilijifanya kutoa onyo.
Mhudumu alichukua ujumbe ule na kumpelekea baada ya kuusoma alijibu:
Nimekuelewa, naomba tuzungumze faragha.
Baada ya kuletewa niliusoma na kumjibu:
Hakuna tatizo.
Baada ya kupelekewa jibu langu, niliona akijadiliana na mpambe wake baada ya muda nilimuona yule mpambe akija nilipokuwa nimekaa na kuniinamia.
“Samahani naomba unifuate.”
“Sawa ngoja nilipe kwanza.”
“Hapana mzee atalipa.”
“Hapana, vinywaji hivi nimeagiza mimi.”
Baada ya kulipa nilitoka na yule mpambe aliyenipeleka mpaka kwenye hoteli moja iliyokuwa nje kidogo ya mji. Moyo wangu ulijawa furaha baada ya kuona mtego wangu umenasa kirahisi tofauti na nilivyofikiria. Jamaa baada ya kunifikisha chumbani aliniacha na kuondoka.
Baada ya kuondoka nilibakia chumbani peke yangu nikiwa katika wakati mgumu wa kutimiza nilicho dhamilia. Wasiwasi wangu ulikuwa kujulikana mimi ndiye muuaji hivyo kunifanya nishikwe mara moja na kukamatwa kabla sijafika mbali.
Nilijikuta nikiingiwa wasiwasi kuhusiana na mpango wangu kwa vile kama ningemuua basi ningekatatwa mara moja. Wazo la kumuua siku ile sikutaka kulitekeleza kwa vile mazingira yalikuwa tata kwa kujua wapambe wake hawakuwa mbali niliamini baada ya kuonekana natoka lazima watamfuatilia na wakimkuta amekufa msako wake ungekuwa mkubwa na mimi nisingefika mbali lazima wangenikamata.
Siku zote niliamini mpango mzuri ni kati yangu na adui yangu asiwepo wa tatu mwenye kujua mpango ule ambaye anaweza kuwa shahidi wa kuweza kunitia hatiani. Nilikubali siku ile nifanye mapenzi tu bila kuingiza kitu chochote huku nikiapa kujituma ili kumfanya aombe tukutane siku nyingine.
Nikiwa katika ya mawazo mkuu wa polisi wa wilaya OCD mzee Mzizire aliingia na kuja moja kwa moja nilipokuwa nimejilaza kwenye kochi.
“Niambie mpenzi wangu?”
“Mmh! Nakusikiliza wewe.”
“Mimi ninalo zaidi ya kuhitaji mapenzi yako.”
“Lakini kweli unanipenda au unanitamani?” nilijifanya kujibalaguza huku nimelegeza macho na sauti.
“Siyo siri mrembo, sijawahi kumpenda mtu kwa haraka hivi kama nilivyokupenda wewe.”
“Muongo! Unanidanganya unataka kunichelea tu leo kisha uniache,” nilijifanya kudeka.
“Kweli kabisa nakupenda kwa dhati wala si kukuchezea.”
“Kweli?”
“Kweli kabisa, unataka nikufanyie kitu gani uamini nakupenda?”
“Unipende tu wala sitaki kitu kingine.”
“Wewe ni mgeni hapa?”
“Ndiyo.”
“Unatokea wapi?”

“ Arusha.”
“Ooh! Vizuri na hapa Morogoro umefikia wapi?”
“Nipo katika mapumziko tu.”
“Unafanya kazi?”
“Ndiyo.”
“Ipi?”
“Kwenye  kampuni ya utalii.”
“Upo likizo?”
“Ndiyo, leo ni siku ya tano, ila kesho nitakuwa Dar ambako nitakaa siku mbili na kwenda Zanzibar kidogo kisha nitaenda Mwanza na kurudi Arusha, kidogo nitakuwa nimeosha macho.”
“Duh! Inaonekama utalii imekukaa sana.”
“Upo ndani ya damu yangu.”
“Kwa nini usimalize likizo yako hapa ili tuwe pamoja, nitakupangia kwenye hoteli hii kwa muda wote utaokuwa hapa.”
“Asante, kwa vile nimeishapanga ratiba zangu, nitakutafutia nafasi yako hata ya kusema uongo kazini kuwa nauguliwa hivyo nitakuja unifiche unifaidi.”
“Basi ondoka kesho kutwa.”
“Hapana naomba kesho uniache niondoke, naweza kuacha kwenda Mwanza nikarudi kwako niache niende Dar na Zanzibar.”
“Mmh! Sawa.”
